MWONGOZO WA KUSAHIHISHA MTIHANI WA KITAIFA 1996
SWALI LA KWANZA

1. **Ufahamu**

a) Mambo manne ambayo ni imani potovu (alama 4)

1. Kuna mbingu na ardhi tu basi
2. Dunia ipo katikati ya maumbile yote
3. Dunia ni tambarare
4. Juu ya ardhi ni mbingu iliyojaa vimulimuli vidogo kulik ardhi
5. Baina ya vimulimuli vipo viwili vikubwa vitwavyo mwezi na jua
6. Mwezi na jua ni vidogyo kuliko ardhi
7. Mwezi ni nyota

b) Maana ya 'Ukweli wa mambo umejitenga kando' 'ni kwamba (alama 2)
Si kweli au
Ukweli untofautiana na imani hii au
Ni kinyume na imani hii

c) Sifa zozote nne za maumbile ya anga (alama 4)

1. Ina rangi ya samawati
2. Mi nusu mviringo
3. Ni kubwa sana
4. Inazidi kupanuka
5. Ndani ya galaksi nyingi ajabu kila uchao
6. Ndani ya galaksi mna nyota nyingi ajabu
7. Nyata ni kubwa sana.
8. Mna sayari tisa zinazolizunguka jua

d) Taja vitu viwili vipatikanavyo katika galaksi (alama 2)
Sayari na nyota au
Miezi au sayari na jua au
Mirihi, mshitara, zalibaki n.k. na jua

e) Sayari mbili ambazo ni kubwa kuliko ardhi ni (alama 2)
Mshitara, zohali, utaridi, sumbla,
Zohali ni sawa na sarateni au zaratani

f) Nyota sio vijitaa vidogo kwa sababu (alama 10)
Jua ni nyota kubwa sana au
Jua ni dogo likilinganishwa na nyota zingine au nyota ni kubwa ajabu

g) Nuru mbili zilizo angani ni. (alama 2)
Nuru ya jua au nyota iliyo asilia nuru ya sayari au miezi kutokana na mmeremeto wa jua

h) i) Neno lenye maana sawa “anga” au “ upeo” ni (alama 1)
Bwaka au
Mbingu

ii) Neno lisilo na maana sawa na paa ni (alama 1)
Tosi

i) Maana ya “mambo pengine ni ya hayo” ni (alama 1)
- Kuwa huenda magalaksi mengine yakawa na viumbe hai…Na pensinge watu pia au
- Huenda magalaksi mengine yakawa na maajabu haya au
- mambo ni sawa nay a ardhi. (Jumla=20)

SWALI LA PILI

2. UFUPISHO:

a) 1. Maisha ya vijana yanaonyesha cheche ya matumaini kwa siku za usoni.
2. Wana sifa za mori na kupenda kujaribu kushika mambo upesi.
3. Upotovu kumawazo na kuiga ambayo ni kipingamizi cha kuendelea kwao kama raia wa kutegemewa. (Zote 3x2=6)

b) 1. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
2. Kiini cha matatizo ya vijana wa leo ni mwongozo na vielezo wanavyopokea katoka kwa walezi/wakuu wao.
3. Wana upotovu wa vyombo vya habari au maandishi na vyombo vya habari.
4. Walezi hufunza wasiyoyatenda au walezi hufanya wasivyosema. Au walezi huhubiri maji na kunywa mvinyo.
5. Jamii na mazingira wanamokulia hutukuza kitu kuliko utu. (Zote 5x1=5)

c) Sifa malezi bora.
1. Kulisha, kuvisha na kuelimisha
2. Kupewa mwongozo unaofaa badala ya kuwanyeshea lawama.
3. Kupewa vielezo vinavyofaa
Jumla ni 17 na kwa utiririko. (Zote 3x2=6)

SWALI LA TATU

3. MATUMIZI YA LIGHA

a) i) Bei ya viatu imepanda juu sana siku hizi. (anaweza kuacha juu)
ii) Weka mizigo katika gari/ ndani ya gari/garini/ juu ya gari /kwenye gari. (alama 2)

b) i) Mikono yao imegusana au kukutana lakini inaweza kutengana kwa urahisi/ushirika wa kaeaida/kusalimiana.
ii) Mikono yao imekwama na vigugu kutengana/imeganda. (alama2)

c) 1) **Usijaribu**
Kupunguza/kushusha/kufifisha/kuteremsha/kuteremsha/dudidimiza sauti unapoimba.

II) Huyu ni mtu mpumbavu/mjinga/jura/juha/nyonge/suzu bwege/pimbi. (alama 1)

III) Binadamu hawezi kumuumba mwenzake

d) 1) Kula uvundo – kutofaidika, kupata hasara, kupata shida, kula mwata. (alama 2)

ii) Kula uhondo-kupata starehe/neema/raha/ufanisi/manufaa/faida/utamu (alama 2)

e) **Kuakifisha**

Bwana mwenyetiti, mgeni wetu wa leo wazazi, walimu wote na hata hat hata wanafunzi.
Leo ni siku muhimu. Au; leo ni siku mujimu.
Je mngependa ua
Je! Mngependa niwafahamishe msaada tulipokea kutoka kwa Wizara ya Elimu?"
(alama 4 x½ kwa kilamoja)

f) **Maana**

Mhariri-anayesoma na kusahihisha au kurekebisha maandishi tayari kwa uchapishaji/kusanifisha/kukosoa).
Jasusi-anayepeleleza habari Fulani (alama 4)

g. i) Ngome hii nzuri/hizi nzuri zinapo

ii) Mitume hawa wazuri wanapendeza
iii) Heshima hii nzuri inapendeza
iv) Ngo'mbe huyu mzuri anapendeza
v) Ngo'mbe hawa wazuri wanapendeza
vi) Vilema hawa wazuri wanapendeza
vii) Vilema hivi vizuri vimependea (alama 5)

h)

	Jina	**kitezi**
i)	Mnada	Nadi
ii)	Kikomo	Koma
iii)	ruhusa	ruhusu
iv)	Ashika/shauku	Ashika
v)	Hsidi/husada	Husudu

(alama 5)

i) i) Mseno halisi
"Ninataka kwenda sokoni" mvulana alimwambia babayeake. Au Mvulana alimwambia baba yake, "Ninataka kwenda sokoni."
"Baba ninataka kwenda sokoni," (alama 2)

ii) Mseno wa taarifa
Kamau alimwambia shangazi yake kuwa angekuwa akienda pale/hapo kila siku kumwona. (alama 2)

j) Po ya kwanza inaonyesha wakati
po ya pili inaonyesha mahali (alama 2)

k) i) alilia Hapo
ii) alifia Hapo
iii) aliolea Hapo
Akiongeza ‘ku’ mkosoe kisarufi (alama 3) Jumla=40.

Jinsi ya kukosoa
Ondoa ½ alama kwa kosa la hijai linapotokea mara ya kwanza hadi jumla ya makosa 6 yaani alama 3.

Ondoa ½ alamu kwa kosa la sarufi linapotokea mara ya kwanza hadi jumla ya makosa 12 kwa upande wa ufahamu na matumizi ya lugha ondoa jumla ya makosa 10 ya sarufi yaani alama 5 kwa upande wa muhtasari.

Usikosoe zaidi ya mara 2 upande wa matumizi mabaya ya herufi kubwa, vilevile herufi ndogo (herufi hizo zapaswa kuwa tofauti).

Mwanafunzi akipata sufuri uadhibu tu upande wa hijai-usiadhibu sarufi. Usiadhibu zaidi ya nusu ya alama alizopata mwanafunzi kwa upande wa sarufi.

Muhtasari
Toa zaidi ya kwanza baada ya maneno 10 (yaani alam 1) kisha uondoe ½ alama kwa kila maneno 5 mfano; mwanafunzi aliyezidisha ufupisho wake kwa maneno 20 ata ondolewa alama 2 lakini aliyezidisha kwa maneno 9 haondolewi alama yoyote (lazima yafike kumi kwanza.).